
# Yesu
# Mkombozi wa Ulimwengu



# YESU MKOMBOZI WA ULIMWENGU

**.......** *'nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao'* **Mathayo 1: 21.**

Kamwe haijawahi kutokea katika historia ya wanadamu kuthubutu kuhitaji Kiongozi mwenye uwezo kama huo. Tunahitaji mmoja mwenye uwezo wa kuongoza mataifa yenye chuki dhidi ya ubinafsi na kuukomesha ili kutuingiza katika mazingira mazuri ya uaminifu na nia njema. Bila hii hapatakuwa na amani au usalama aidha kwa mtu mmoja mmoja wala taifa.

Kuna mashujaa wengi ambao majina yao na mafanikio yao hutukuza kurasa za kihistoria. Lakini hakuna hata mmoja wao aliyekabiliana na hali ngumu sana kama ilivyo hivi sasa katika Dunia,wala hapakuwa na matatizo mengi sana. Leo hii kila taifa lina matatizo na hakuna anayeonekana kutafuta suluhu kamilifu. Ulimwengu unamuhitaji shujaa, ili kuindoa dunia kwenye machafuko ambayo yametengenezwa katika vita ya kwanza na ya pili ya dunia.  Lakini tutampata wapi shujaa kama huyo? Hakuna anayejaribu kuongelea.

Katika biblia, Muumbaji amewapa mpango kazi wake kwa ajili ya amani ya Dunia. Maneno yake yanaonesha wazi kwamba Yesu ni moja kati ya mpango mtakatifu kwa ajili ya baraka ya watu. Nyimbo za Malaika katika usiku wa kuzaliwa Yesu ni tosha kuonesha hili, kwa maana walimtambua kama mkombozi wa Ulimwengu, ambaye kupitia kwake nia njema ya Mungu ingedhihirika kwa watu wanaokufa. Malaika hao pia walitabiri kuwa kupitia Yesu amani ingekuja Ulimwenguni.

Lakini Yesu ni nani na zipi sifa zake? Tuna sababu gani kwa kuamini anasifa zote za kuleta amani kwenye ulimwengu wenye machafuko? Tunajua hakuna njia bora ya kutafuta majibu ya maswari haya zaidi ya kuchunguza nabii na ahadi katika neno la Mungu ambalo linamuongelea yeye na sifa zake. Tunapofanya hivi ,mpango wa Mungu wenyewe, unavyomuhusisha

Yesu, mtoto wake, itafunuliwa kwetu katika utukufu wa upatano na uzuri wake.

## NENO(LOGOS) AKAFANYIKA MWILI

Yesu alikuwepo kabla hajawa mwanadamu. Hoja hii inawekwa wazi katika ***Yohana 1:1-3*** :Katika ***Yohana 1:14*** tunasoma kwamba *'..naye neno akafanyika mwili,akakaa kwetu, nasi (tukauona utukufu wake kama wa mwana pekee atokaye kwa Baba) amejaa neema na kweli'* kwamba neno(logos—mwanzo) akafanyika mwili, kwamba alitolewa kwenye hali yake aliyokuwa nayo kabla na kuwekwa kwenye hali ya Ubinadamu, imefunuliwa katika Biblia kuwa kipengele cha msingi katika mpango wa Mungu. ***Waebrania 2:9,14*** inasema hii ilikuwa ili afe kama mwanadamu kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.

Katika ***Yohana 6:51*** tunapata maelezo ya mwenyewe kuhusu hili, na alisema alipaswa kuutoa mwili wake kwa ajili ya uhali wa ulimwengu. Hii sadaka ya ubinadamu wa Yesu ulikuwa kama mbadala kwa maisha yaliyopotea katika Baba Adamu. Paulo anathibitisha hili kwamba *'Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa'* **1Wakorinto 15:22** Katika 1Timotheo 2:6 mtume anaeleza kwamba alijitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya wote, neno Fidia kwa kigiriki imetafsiriwa kumaanisha 'gharama inayolingana'

Hapa, basi, ni falsafa ya mpango wa Mungu wa ukombozi kupitia Kristo. Mwana wake wa pekee alifanywa kuwa mwili mkamilifu—ili apate kuwa badala ya kifo cha Adamu aliyehukumiwa, na hivyo kuandaa njia ya kuepushwa na kifo kwa ajili ya Adamu na jamii yake yote. Ndivyo Yesu alivyokufa kwa ajili ya wanadamu wote.

Ulimwengu mzima husifu roho ya dhabihu kwa niaba ya wengine, na kutambua thamani yake kwa wale ambao wangetawala juu ya watu. Wote wanajua ubaya unaotokana na mtawala kutafuta tu masilahi yake mwenyewe, ustawi wake, maendeleo yake mwenyewe,

na ongezeko la mamlaka yake mwenyewe, bila kujali jinsi wengine wanavyoweza kuathiriwa. Labda moja ya sifa zinazosifiwa sana, zinapokuwa na wale wanaojaribu kusimamia mambo ya serikali, ni utayari wa kutumia na kutumiwa kwa maslahi ya watu.

Lakini katika masimulizi yote ya historia, hakuna mtawala, mtu wa-serikali, Rais, Mfalme, Malikia, au dikteta ambaye amewahi kufanana na Yesu katika roho yake ya ujitoaji, kwanza kwa Mungu na kisha wanadamu. "*Alienda huku na huko akitenda mema,"* Maandiko yanatuambia. (Matendo ya mitume 10:38) Alitumia nguvu zake kuwafundisha wengine, kila siku alipoendelea na huduma yake ya kujidhabihu. Na hatimaye akamaliza maisha yale ya ajabu ya utumishi kwa kujitolea kwa hiari yake kifo hicho cha kikatili pale msalabani.

Hivyo ndivyo mwanadamu Kristo Yesu alivyothibitisha uaminifu wake. Ulimwengu utaweza kumwamini mtu huyo mtukufu wanapojifunza juu yake wakati ufalme wake ambao ameahidiwa muda mrefu utakaposimamishwa duniani na kutawala kama serikali ya ulimwengu kwa ajili ya baraka za watu.

## KUHANI NA MFALME

Jina Yesu linamaanisha yule anayeokoa - mwokozi. Lakini mpango wa Mungu wa kuuokoa ulimwengu kutoka katika dhambi na mauti ni mpana sana kana kwamba ili kutusaidia kuelewa maana yake yote, Mungu, kupitia Neno lake, amempa Yesu majina mengi na vyeo tofauti tofauti, kila moja likitoa maana fulani hususa kuhusu wokovu unaoletwa na Yesu kwa watu wafao. Moja ya majina haya ni "kuhani"

Tunapofikiria cheo hiki cha "kuhani" hatupaswi kuweka akilini namna ya matumizi mabaya ya neno hili kama makundi mbalimbali ya madhehebu, lakini tunapaswa kurudi kwenye Agano la Kale na kuona umuhimu unaohusishwa na matumizi yake ya awali. Mungu aliweka makuhani ili kutumikia taifa la Israeli katika mambo ya ibada. Kazi zao zilikuwa mbili -

walitoa dhabihu, na kisha wakaeneza baraka kwa watu, kulingana na toleo la dhabihu,

Ndivyo ilivyo kwa Yesu. Tayari ametumikia akiwa kuhani kwa ajili ya toleo la dhabihu, na baadaye ataeneza ulimwenguni baraka ya uzima wa milele, inayopatikana kwa sababu ya dhabihu aliyotoa. Kwa habari ya makuhani wa Israeli, walitoa wanyama katika dhabihu ya mfano, lakini Yesu alijitoa mwenyewe kuwa dhabihu kuu ya ufananisho.

Yesu pia ameteuliwa na Mungu kuwa Mfalme wa dunia, na katika Waebrania 6:20 ; 7:1, 2 mtume anaunganisha ofisi hizi mbili katika nafsi ya Yesu. Hivyo tunakumbushwa kwamba atatawala watu na kuwabariki. Kuhusu Mfalme huyu wa kikuhani nabii aliandika:

"Naam, wafalme wote na wamsujudie; Na mataifa yote wamtumikie. Kwa maana atamkomboa mhitaji aliapo, Na mtu aliyeonewa iwapo hana msaidizi. Atamhurumia aliye dhaifu na maskini, Na nafsi za wahitajiataziokoa. Atawakomboa nafsi zao na kuonewa na udhalimu, Na damu yao ina thamani machoni pake. "— Zaburi 72:11-14

Unabii wa namna hii unaweza kuthaminiwa tu katika nuru ya ahadi ya Mungu kwamba Yesu atatawala juu ya dunia kwa miaka elfu moja. Si suala la kusubiri watu wakubali ufalme wake ndipo aweze kutawala. Kuna wakati dhahiri katika mpango wa Mungu kwa Ufalme kusimamishwa duniani. Katika unabii fulani kuhusu Yesu akiwa Mfalme mpya wa dunia, tunaambiwa kwamba kwanza atayavunja-vunja mataifa kama "*chombo cha mfinyanzi*" - Zaburi. 2:5-12.

## JAJI/HAKIMU

Cheo kingine ambacho Maandiko yanampa Yesu ni "Hakimu" Kama hakimu yeye pia atakuwa baraka wa watu. Mtunga-zaburi aliandika hivi kumhusu Yesu, "Atawahukumu walioonewa wa watu, Atawaokoa wahitaji, atamseta mwenye kuonea" ( Zaburi 72:4 )

Shetani, Ibilisi, ndiye mkandamizaji mkuu wa watu kwa nyakati zote. Amezifanya akili za watu kuwa watumwa kwa njia ya udanganyifu, na hivyo kuwazuia wasimjue na kumtumikia Mungu wa kweli, ambaye kumjua na kumtumikia kwa njia ifaayo kutamaanisha uhai wa milele.

Maoni yasiyo sahihi ya kimapokeo kuhusu siku ya hukumu yamewazuia wengi wasimthamini Yesu kuwa Jaji mkuu wa wanadamu. Badala ya kuitazamia siku ya hukumu kuwa wakati wa baraka, wameogopa kuikaribia, wakidhani kuwa ni wakati wa maangamizi karibia kila mtu. Kwa kweli, ile miaka elfu ambayo Yesu 'atahukumu ulimwengu katika uadilifu' itakuwa wakati wa baraka kwa watu. — Matendo 17:31.

Wazazi wetu wa kwanza walipovunja sheria takatifu, wakajileta wao wenyewe na wazao wao chini ya hukumu ya kifo. Lakini kifo cha Yesu akiwa Mkombozi wa wanadamu kiliandaa njia ya kuepuka hukumu hiyo. Faida zinazopatikana kutokana na kifo cha Yesu zinapatikana tu kwa kumwamini, na kutii mapenzi ya kimungu. Lakini Paulo anaibua swali, "Watamwaminije yeye ambaye hawakusikia habari zake?" ( Warumi 10:14 ) Ni watu wachache ambao wamesikia habari za Yesu kwa njia kamili inayohitajiwa ili wamwamini. Lakini Maandiko yanaonyesha kwamba watapata fursa hiyo katika siku ya hukumu inayokuja.

Kwa hiyo siku ya hukumu itakuwa ni wakati wa nuru kwa watu. Paulo anadokeza hili katika mahubiri yake kwenye kilima cha Mars, ambamo analinganisha "nyakati za ujinga huu" na siku ambayo Mungu ameiweka ambapo "atauhukumu ulimwengu kwa haki kwa mtu yule aliyemweka," Yesu Kristo. Mwenye Haki. ( Matendo 17:31 ) Huo utakuwa "wakati ufaao" ambapo uhakika mkuu wa kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu 'utashuhudiwa,' au kujulishwa, kwa wanadamu wote. - 1Timotheo. 2:4-6.

Kwamba kazi ya hukumu itahusisha kuwaangazia watu kama inavyoonesha katika Ufunuo 20:12 , ambapo tunaambiwa kwamba "vitabu" vitafunguliwa na kila mtu

atahukumiwa kulingana na mambo “yaliyoandikwa katika vitabu” wengine kimakosa wanadhani kuwa vitabu hivi vina kumbukumbu za maisha ya zamani ya jamii ya wanadamu, na kufunguliwa kwa vitabu hivyo kunaashiria kwao kwamba dhambi na mazuri yao yatapitiwa katika siku ya hukumu, na hivyo kuwa kuhukumiwa kustahili au kutostahili uzima wa milele.

Lakini hakuna chochote katika Maandiko kuthibitisha hitimisho hili. Maandiko haya yanasema watu watahukumiwa kwa mambo yaliyoandikwa katika vitabu hivyo, na Yesu alisema kwamba “neno” lake litawahukumu watu wakati huo. ( Yohana 12:48 ) Kufunguliwa kwa vitabu hivi vya alama lazima kumanishe ufunuo wa ukweli kama kiwango cha hukumu.

Katika Isaya 29:11, 12 wazo kama hilo linaletwa kwetu. Hapa "kitabu" kinajadiliwa. Ni kitabu "kilichotiwa muhuri", ambacho hakiwezi kufunguliwa ama na wenye elimu au wasio na elimu. Lakini unabii unaonyesha kwamba hatimaye kitabu hiki chafunguliwa, na kuwawezesha viziwi na vipofu kusikia na kuona yaliyoandikwa humo. Unabii huu unatukumbusha juu ya giza la kiroho ambalo linawafunika watu kwa utawala wa dhambi na mauti, na unatuhakikishia kwamba wakati utakuja ambapo giza hili litaondolewa. Ndipo watu wataona na kujua mapenzi ya Mungu.

Ni siku hii ya wakati ujao ya mwangaza ambayo Biblia hutaja kama siku ya hukumu, ambayo Yesu atahukumu ulimwengu kwa uadilifu. Hautakuwa wakati wa kutoa tu tuzo na kutamka hukumu. Kazi ya hukumu inajumuisha mtihani chini ya mwangaza ambao utawapata wakati huo.

Hii itakuwa nafasi ya kwanza kabisa ya kweli na kamili ambayo ulimwengu utakuwa umepata kwa kumwamini Kristo na kupokea uzima wa milele. Wote walikuja chini ya hukumu kupitia Adamu, na walio wengi sana wanaingia kaburini bila hata kujua kwamba Kristo alikufa kwa ajili yao. Lakini wakati wa siku ya hukumu, wataamshwa kutoka mautini, wakiangaziwa juu ya Yesu

na, kwa msingi wa nuru hiyo, watapewa fursa ya kukubali zawadi ya Mungu, kutii sheria za ufalme, na kuishi milele.

## MSHAURI WA AJABU

Isaya 9:6, 7 ni unabii wa ajabu wa kuzaliwa kwa Yesu na upeo wa ulimwenguni pote wa serikali ambayo atasimamia. Ili kutusaidia kufahamu kikamili zaidi jinsi uharibifu wake utakavyomaanisha kwa watu, Unabii huu unampa majina kadhaa yenye maana. "Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani"

Baadhi ya wasomi wa Kiebrania wanadai kwamba hakuna alama za uandishi zinazopaswa kufuata neno “Ajabu,” kwamba ni kivumishi tu cha “mshauri” Bila shaka, tunajua kwamba Yesu ni “Waajabu” Haijalishi tunamwona Bwana kwa maoni gani, yeye ni “Ajabu" Lakini inaonekana kwamba hapa Bwana anatuambia kwamba Yesu ni "Mshauri wa Ajabu."

Neno hili "Mshauri" linamaanisha zaidi ya yule anayetoa ushauri: ni kama neno wakili wetu, anayemwakilisha mteja mbele ya mahakama. Yesu atatenda katika nafasi hii atakapotumika kama “Mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu” (1 Tim. 2:4-6) Kazi yake kama Mshauri itakuwa sawa na jukumu lake kama hakimu. Katika mambo yote mawili atashughulika na watu ili kutimiza upatanisho wao pamoja na Mungu, na hivyo kuwaandalia uhai udumuo milele.

Kwa kweli Yesu atakuwa “Mshauri wa Ajabu” na hakimu mwadilifu. Katika unabii mwingine tunasoma juu ya hakimu huyu wa wakati ujao, “Na roho ya Bwana atakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uweza, roho ya maarifa na ya kumcha Bwana; na furaha yake itakuwa katika kumcha Bwana; wala hatahukumu kwa kuyafuata ayaonayo kwa macho yake, wala hataonya kwa kuyafuata ayasikiayo kwa masikio yake; bali kwa haki atawahukumu maskini, naye atawaonya wanyenyekevu wa dunia kwa adili; naye

ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake, na kwa pumzi ya midomo yake atawaua wabaya”- Isaya. 11:2-4.

Mwenye aliye na sifa hizo atashughulikia watu kwa haki, na chini ya usimamizi wake wale wanaotamani kumrudia Mungu na kupokea baraka ya uhai wa milele katika dunia iliyokamilishwa watapewa kila nafasi ya kufanya hivyo.

Uhakika wa kwamba hatahukumu baada ya kuona kwa macho, wala kwa kusikia kwa masikio ni muhimu sana kujua. Waamuzi wenye uwezo mkubwa kuliko wote ambao ulimwengu umewahi kuwa nao wamekuwa na kikomo katika kufanya maamuzi yao juu ya kile kinachoweza kuonekana na kusikilizwa wameshindwa kutazama ndani ya mioyo ya watu na kugundua nia zao zilizofichika, au kama maneno na matendo yao. yalikanusha ukweli halisi wa maisha yao. Lakini Yesu atapewa uwezo wa kimungu wa utambuzi. Atajua ukweli kuhusu wote, bila kujali taaluma zao. Si ajabu kwamba Paulo alisema kwamba ulimwengu utahukumiwa kwa haki na mtu yule ambaye Mungu amemweka! —Matendo 17:31.

## MUNGU MWENYE NGUVU.

Jina lingine linalotolewa kwa Yesu ni ‘Mungu Mwenye Nguvu’ ( Isaya. 9:6 ) Hilo halimaanishi kwamba Yesu ni “Mungu Mweza-Yote,” bali linamaanisha kwamba ameinuliwa sana katika mpango wa kimungu na kwamba Muumbaji anafurahi kumtambua kama Mungu Mwenye Nguvu na kuabudiwa Katika Yohana 5:22, 23 tunajifunza kwamba Baba wa Mbinguni amekabidhi hukumu yote kwa Mwana wake, na kwamba anatamani watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu yeye.

Katika Isaya 53:12 nafasi ya juu ya Yesu katika mpango wa kimungu inaletwa kwetu tena. Katika sura hii mateso na kifo cha Mkombozi wa ulimwengu vimetabiriwa. Kwa sababu ya uaminifu wake Muumba anaahidi, “Kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu” Hili lilitimizwa wakati Yesu alipofufuliwa kutoka kwa wafu

na kuinuliwa sana hadi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. Huko akawa “Mungu mwenye nguvu,” Yule ambaye ulimwengu mzima unaweza kumtegemea kwa msaada, na kutoka kwake, kama mwakilishi wa Muumbaji, wanaweza kutarajia baraka za wokovu kutoka katika dhambi na mauti.

Unabii mwingine kuhusu Yesu ulitabiri kwamba jina lake litakuwa ‘Immanueli,’ ambalo linamaanisha, ‘Mungu pamoja nasi’ (Isaya. 7:14). Hii haimaanishi kwamba Yesu ni Mungu Mwenyezi, Muumbaji mwenyewe, bali kwamba atakuwa mwakilishi wa Mungu. Kuja kwa Yesu duniani kufa kwa ajili ya watu kulikuwa udhihirisho wa ajabu wa upendo wa Mungu. (Yohana 3:16). Miujiza yake ilikuwa mfano mzuri wa nguvu alizopewa na Mungu, ambazo zitatumiwa na Kristo aliyefufuka kwa ajili ya kuponya wagonjwa wote na kufufua wafu wote.

Maandiko hushuhudia kwamba kwa habari ya utu wa Yehova Muumba, hakuna mwanadamu anayeweza kumuona na akaishi. ( Kutoka. 33:20 ) Lakini katika Yesu wanadamu waliona sifa tukufu za Mungu zikidhihirishwa. Na kupitia sheria za ufalme wake watatambua hata zaidi kwamba kupitia yeye haki, hekima, upendo, na nguvu za Mungu Mweza-Yote zimeanza kutumika kwa ajili ya baraka zao za milele. Kwa furaha, basi, watu watamtambua Yesu kuwa mwakilishi wa Mungu, na udhihirisho wa kuwapo kwa Mungu katikati yao.

## MIKAELI ATASIMAMA

Katika Danieli 12:1 jina linguine linatumika kwa Yesu, ni, “Mikaeli” Neno Mikaeli kihalisia linamaanisha “aliye kama Mungu”—yaani, mtu anayetenda kama mwakilishi wa Mungu. Katika unabii huu tunasoma kwamba "Mikaeli atakapo simama" kutatokea "wakati wa taabu, ambao haujawahi kutokea tangu kuwepo kwa taifa." Kwa maneno mengine, jina hili linafafanua kuhusiana na kupindua falme za ulimwengu huu, kutayarisha kusimama kwa utawala wake wa uadilifu duniani.

Tumezoea kumfikiria Yesu kuwa mwenye fadhili na amani. Lakini udhihirisho wa mamlaka yake na uwezo wake juu ya uovu na mamlaka mbovu za dunia utaleta taabu - " wakati wa taabu ambao haujawahi kutokea tangu lilipoanza kuwapo taifa." Hata sasa tunashuhudia mwanzo wa shida hii, inayotarajiwa kuja juu ya mataifa ya dunia mwishoni mwa enzi. Hata katika unabii wa Isaya 11:2-9 , ambapo tunasoma kwamba Yesu atawahukumu maskini kwa haki, pia inatangazwa kwamba "kwa pumzi ya midomo yake atawaua waovu".

Itakuwa kwa sababu ya ukamilifu wake katika kuondosha uovu wote na watenda maovu wote duniani ndipo hatimaye amani na utulivu vitakuja kwa watu. Hali ya ulimwengu mzima ya furaha na nia njema itakayofuata kuangamizwa kwa maadui wa Mungu wakati wa utawala wa Kristo-hata mauti yenyewe (1Kor. 15:26) - inaonyeshwa katika unabii na wanyama mbalimbali wa dunia wataishi pamoja kwa amani. . "Mbwa-mwitu atakaa pamoja na mwana-kondoo, na chui atalala pamoja na mwana-mbuzi; ... na mtoto mdogo atawaongoza." — Isaya 11:6.

## BABA WA MILELE

Isaya anatangaza kwamba Yesu pia atakuwa "Baba wa milele." Hii haimaanishi, hata hivyo, kwamba yeye ndiye ambaye sisi, kama Wakristo, tunamwita "Baba yetu wa Mbinguni" Neno baba linamaanisha mpaji wa uzima, na baba wa milele angekuwa yule anayetoa uzima wa milele. Yesu atafanya hivyo kwa wale wote ambao, wakati wa miaka elfu ya utawala wake, watamwamini na kutii sheria ya ufalme wake. Uhai waliopokea watu kutoka kwa baba zao wa asili umekuwa wa muda mfupi na usio na uhakika, lakini wote wanaokuja kwa Yesu wakati huo watapewa uzima wa milele.

Andiko lingine linalotupa nuru juu ya mpango wa kimungu wa kuwapa watu uhai kupitia Yesu ni 1 Wakorintho 15:45, 47 . Hapa mtume anamwelezea Yesu kuwa "Adamu wa mwisho," na anatangaza kwamba katika ufufuo wake kutoka kwa wafu alifanywa

kuwa “roho inayohuisha [itoayo uhai]; yaani roho iliyopewa uwezo wa kuwapa wengine uhai.

“Mtu wa kwanza [Adamu]” alikuwa wa dunia, wa udongo. Yeye na mke wake waliamrishwa wazae na waijaze dunia kwa uzao wao. Hivyo akawa baba wa kwanza wa jamii ya wanadamu. Hata hivyo, kwa sababu alivunja sheria ya kimungu, alijiletea hukumu ya kifo. Hivyo ilikuwa kwamba “mtu wa kwanza Adamu” alizaa jamii katika hali ya kufa.

Lakini itakuwa tofauti kwa Adamu wa mwisho. Adamu wa mwisho atazaa upya watoto wa Adamu wa kwanza na kuwawezesha kufurahia uzima wa milele. Hivyo atakuwa “Baba wa milele.” Na Yesu mwenyewe alirejelea Ufalme wa Milenia kuwa wakati wa "kuzaliwa upya" - Mathayo 19:28

Kwa kupatana na hili, unabii wa Isaya 53:10 unatuambia kwamba Yesu ataona “uzao” wake Mstari wa nane wa sura hii unazungumza juu ya kukatiliwa kwake mbali na nchi ya walio hai, na kusema kwamba hapakuwa na yeyote wa kutangaza kizazi chake. . Yaani, hakuoa na kulea familia kama wanaume wanavyofanya kwa kawaida, kwa hiyo hakuna wazao wa asili wa Yesu, hakuna wa "kutangaza kizazi chake."

Hata hivyo nabii anasema, "Atauona uzao wake"; yaani, watoto watalelewa kwake—si kwa njia ya kawaida, bali kwa sababu ya ukweli kwamba akiwa Mkombozi wa ulimwengu atakuwa katika nafasi ya kuwapa watu uhai. Yeye ndiye atakayewapa uhai au baba yao. Na kwa sababu hiyo, Yesu “ataona taabu ya nafsi yake, na kuridhika.” – Isaya 53:11

"Utungu" unahusishwa na kuzaa watoto, na hapa nabii anatumia neno kwa njia ambayo Yesu huwapa watu uzima. Uchungu huu unafafanuliwa waziwazi katika sura ya 53 ya Isaya. “Alidharauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko.” Pia, aliongozwa “kama mwana-kondoo aende kuchinjwa,” na pia kuteswa na kuteswa.

Ndiyo, huu ulikuwa ni utungu kweli kweli, ambao uliendelea pamoja naye hadi msalabani, ukiisha tu wakati, kutoka kwa moyo wake uliyopasuka, alilia "Imekwisha." Lakini kutoka kwa utungu huu utatoka maisha ya kuzaliwa upya kwa Adamu wote wa kwanza. watoto ambao wataikubali kwa masharti ya imani na utii. Hivyo Yesu "ataona taabu ya nafsi yake, na kushibishwa," kwa maana mamilioni yasiyohesabika watamsifu kuwa baba yao, mtoa uhai wao, na kwa nia moja wataimba sifa zake, wakisema, "Tutashangilia na kushangilia wokovu wake" Msifu Mungu kwa zawadi yake kwa wanadamu wa "Baba wa milele".

## MFALME WA AMANI

Yesu, Mwokozi wa ulimwengu, atakuwa pia "Mfalme wa Amani." ( Isaya 9:6 ) Wimbo wa malaika ambao ulitangaza kuzaliwa kwa Yesu unaweka hali ya furaha yaa "amani duniani," na hatimaye amani hiyo itakuwa halisi. Yesu atakuwa Mfalme mkuu ambapo "mlima" - ufalme - wa Bwana "utaimarishwa juu ya milima, na ... utainuliwa juu ya vilima" ( Mika 4: 1 ) Wakati mataifa ya dunia yanapotambua usemi huo. kushindwa kwa juhudi zao wenyewe za kusimamisha amani badala ya dhiki ya sasa watasema, "Njoni, twende juu mlimani (Ufalme) wa Bwana ... naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda. katika njia yake"—Mika 4:2

Wakati mataifa yatakapo tafuta njia za Bwana hivyo na kuwa tayari kutembea katika njia hiyo, 'watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu,' na "taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifunza vita kamwe" ( Mika 4:3 ) Hivyo Mfalme wa Amani ataleta amani kati ya mataifa.

Lakini atafanya zaidi ya kuanzisha amani kati ya mataifa. Hili bado lingeacha ugomvi na machafuko ndani ya mataifa. Yesu ataleta amani ya ulimwenguni pote, ambayo itamaanisha amani kati na ndani ya mataifa—amani ya jumuiya, amani ya familia, na muhimu zaidi, amani ya moyo.

Amani hii ya moyo itatokana na kuwa na amani pamoja na Mungu. Ulimwengu wa leo umetengwa na Mungu kupitia matendo maovu. ( Efeso. 4:18, 19; Kolosai. 1:21 ) Lakini yule Mkuu wa Amani, akitumikia akiwa Mpatanishi, Mshauri, na mwamuzi, atawapatanisha wanadamu na Mungu. Jamii ya wanadamu haitakuwa tena katika uasi dhidi ya Muumba. Na wakiwa katika upatano naye na kufurahia mwanga wa jua wa upendeleo wake, watapata uzima wa milele. - Zaburi 30:5

## KWA MWANAKONDOO MILELE

Yesu, Mwokozi wa ulimwengu, anaonyeshwa katika Ufunuo 5:6, 11-13 kama Mwana-Kondoo aliyechinjwa. Maelezo haya ya alama(symbolic) ya Yesu yanarejelewa mara nyingi katika Maandiko. Katika sura ya 53 ya Isaya limetumiwa sana katika unabii wa kuteseka na kifo cha Yesu. Mtume Petro anaeleza kwamba unabii haukutabiri tu kuteswa kwa Yesu, bali pia "utukufu utakaofuata" ( 1 Petro 1:11 ), na katika Ufunuo 5:13 maelezo mazuri ya utukufu wake uliotabiriwa yanawekwa wazi. Tunanukuu:

"Na kila kiumbe kilichoko mbinguni na juu ya nchi na chini ya nchi ya juu ya bahari, na vitu vyote vilivyomo ndani yake, nalivisikia, vikisema, Baraka na heshima na utukufu na uweza una yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na yeye Mwana-Kondoo, hata milele na milele"

Hapa kuna ishara ya upatanisho mkamilifu wa kukumbatia yote kwamba "kila kiumbe" kitaimba sifa za Mungu na za Mwana-Kondoo. Hii haimaanishi wokovu wa watu wote bila kujali imani au utii, kwa maana unabii mwingine unasema wale ambao hawatatii "wataangamizwa kutoka miongoni mwa watu." ( Matendo 3:19-23 ) Lakini inamaanisha wale wanaokubali fursa katika ufalme. watarejeshwa kwenye upatano na Baba, na watamheshimu Mungu na Mwana wake mpendwa, Mwokozi wetu.

## PAMOJA NA MWANAKONDOO

Mwana-Kondoo aliyechinjwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu na sasa ameinuliwa yupo mkono wa kuume wa Mungu ili awe Mfalme wa dunia – " simba wa kabila la Yuda" ( Ufunuo. 5:5; Mwanzo. 49:9 ). - baadaye katika Kitabu cha Ufunuo kilichoonyeshwa kama amesimama juu ya Mlima Sayuni. ( Ufunuo. 14:1 ) Hiyo ni ishara ya mamlaka yake ya kifalme na kuinuliwa kwake. ( Zaburi 2:6-9 ) Katika picha hii ya Mlima Sayuni tunaambiwa kwamba wengine watakuwa pamoja na Mwana-Kondoo katika cheo hicho kilichotukuka sana kinachowakilishwa kuwa 144,000.

"Hawa ndio," twasoma, "wamfuatao Mwana-Kondoo kokote aendako." ( Ufunuo :14:4 ) Hawa ndio wale wale wanaorejelewa katika Ufunuo 20:4 , ambao walidhabihu uhai wao "kwa ajili ya ushuhuda wa Yesu, na kwa ajili ya Neno la Mungu" Kwa sababu hiyo "waliishi na kutawala pamoja na Kristo miaka elfu moja" Hawa ndio waliotajwa na Mtume Paulo kuwa "watoto wa Mungu," na "ikiwa ni watoto, basi warithi; warithi wa Mungu, na washirika wao pamoja na Kristo." — Warumi 8:16, 17

Hawa, kwa ufupi, ***ni kanisa la kweli la Kristo,*** linaloitwa kutoka katika ulimwengu wakati wa sasa. Kwa ajili ya kuyatoa maisha yao kwa uaminifu katika huduma ya kiungu, watashiriki ufalme heshima na utukufu pamoja na Yesu. Watatawala pamoja naye kama makuhani na wafalme. ( Ufunuo 20:6 ) Watakuwa waamuzi pamoja naye. ( 1 Wakorintho. 6:2, 3 ) Wanatumikia pamoja naye wakiwa "wahudumu wa upatanisho." ( 2 Wakorintho. 5:18 ) Kwa ufupi, watashiriki heshima ya juu ya vyeo vyote vya juu vya Yesu katika mpango wa kimungu wa kupatanisha ulimwengu uliopotea kwa Mungu. Watashiriki hata makao yake ya mbinguni. — Yohana 14:1-3

Kama "bibi-arusi" wa Kristo, kanisa pia litashiriki katika kazi hiyo tukufu ya wakati ujao ya kutoa uhai na ukamilifu wa akili na mwili kwa jamii inayokufa. "Roho na *bibi-arusi* wasema, Njoo," Mtu wa ufunuo aliandika, "na ayatwae maji ya uzima bure. Ni tazamio tukufu kama nini! — Ufunuo 22:17

Katika Isaya 11:1 Yesu anaitwa “shina la Yese” (baba wa Daudi) lakini katika Ufunuo 22:16 Yesu anaitwa “mzizi” na “mzao” wa Daudi. Kwa kadiri maisha ya kibinadamu ya Yesu yalivyohusika, alikuwa mzao wa Daudi, “shina” Lakini katika nafasi yake ya Mwokozi na Mtoa Uhai anakuwa “mzizi” wa Daudi, yaani, chanzo cha uhai wake. Na si Daudi tu, bali wanadamu wote, watapata fursa ya kufurahia uhai udumuo milele unaopatikana kupitia kazi ya ukombozi ya Yesu.

**Maswari kujikumbusha juu ya japisho hili...**

Neno (Logos) Akifanyika Mwili

1. a.) Yesu alikuwa na jina gani alipokuja ulimwenguni? Eleza Waebrania 2:9

b.) Neno “fidia--ransom” linamaanisha nini?

c.) Je, maana hii inaelezeaje mpango wa ukombozi kupitia Kristo?

Kuhani na Mfalme

2. a.) Je, Yesu anatimizaje kazi ya ukuhani?

Hakimu/Mshauri wa ajabu

3. a.) Siku ya hukumu ni nini?

b.) Nini kitatokea wakati huo?

Mungu Mwenye Nguvu

**4.** a.) Je, “Mungu Mweza Yote” ni sawa na “Mungu mwenye nguvu” wa Isaya 9:6 ?

b.) Elezea kila moja.

Michael Atasimama

**5. a.) “Mikaeli” katika** Danieli 12:1 ni nani ?

b.) Anafanya nini?

Baba wa Milele

**6.** a.) Je, Yesu na Baba yetu wa mbinguni ni mtu mmoja?

b.) Ni nini basi kinachomaanishwa na fundisho la Biblia kwamba Yesu atakuwa “baba wa milele”?

Baba wa Milele

**7.** a.) “Adamu wa kwanza” na “Adamu wa mwisho” ni akina nani?

b.) Kila mmoja anafanya nini?

Kwa Mwanakondoo Milele / Pamoja na Mwana-Kondoo

**8.** a.) Katika Ufunuo 14:1 Mwanakondoo ni nani?

b.) Wale 144,000 walio pamoja naye ni akina nani?

Pamoja na Mwanakondoo

**9.** a.) Kanisa la kweli la Kristo ni lipi?

b.) Kazi yao itakuwa nini?

**10.** a.) Ni nani atakayemtambua Bwana kwanza atakaporudi duniani?

b.) Watamtambuaje?